

HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO.

MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 17/12/2021.

WAJUMBE WALIODHURIA:

- | | | |
|---------------------------------|------------------------------------|--------------|
| 1. Mh. Juma Pandu. | - Diwani wa Kata ya Mkongo Gulioni | - Mwenyekiti |
| 2. Mh. Lucas Jacob Njogopa | - Diwani wa Kata ya Rwinga | - Mjumbe |
| 3. Mh. Isdory Nyati | - Diwani wa Kata ya Limamu | - Mjumbe |
| 4. Mh. Grace Kapinga | - Diwani wa Kata ya Magazini | - Mjumbe |
| 5. Mh. Selina Kayombo | - Diwani Viti Maalumu Namtumbo | - Mjumbe |
| 6. Mh. Remna Nchimbi | - Diwani wa Kata ya Msindo | - Mjumbe |
| 7. Mh. Charles Wilbadi Chengula | - Diwani wa Kata ya Kitanda | - Mjumbe |
| 8. Mh. Reginbert B. Henjewele | - Diwani wa Kata ya Hanga | - Mjumbe |

WAJUMBE WASIODHURIA KWA TAARIFA:

- | | | |
|-----------------------|----------------------------|----------|
| 1. Mh. Vita R. Kawawa | - Mbunge Jimbo la Namtumbo | - Mjumbe |
|-----------------------|----------------------------|----------|

WATAALAM WALIOHUDHURIA:

- | | | |
|------------------------------|--|-----------|
| 1. Bw. Chiriku H. Chilumba | - Mkurugenzi Mtendaji (W) | - Katibu |
| 2. Bw. Aden. H. Nchimbi | - Katibu Tawala (W) | - Mtaalam |
| 3. Bi. Neema Msovela | - Kaimu Afisa Utumishi na Utawala (W) | - Mtaalam |
| 4. Bw. Bakari Nihuka | - Kaimu Mweka Hazina (W) | - Mtaalam |
| 5. Bw. Ambokile Paul | - Afisa Mifugo na Uvuvi (W) | - Mtaalam |
| 6. Bw. Geoffrey Kalikawe | - Mtendaji wa Mamlaka M/Mdogo Namtumbo | - Mtaalam |
| 7. Bw. Edwin Swai | - Afisa TEHAMA | - Mtaalam |
| 8. Bw. Jackson Mateso | - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W) | - Mtaalam |
| 9. Bw. Peres Kamugisha | - Afisa Maendeleo ya Jamii (W) | - Mtaalam |
| 10. Bw. Emmanuel Gwao | - Afisa Ushirika (W) | - Mtaalam |
| 11. Bw. Venance Hanje | - Afisa Sheria (W) | - Mtaalam |
| 12. Bw. Andrew Tarimo | - Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika (W) | - Mtaalam |
| 13. Bw. Amos Kanige | - Afisa Mipango (W) | - Mtaalam |
| 14. Bw. Protas Komba | - Afisa Elimu Msingi (W) | - Mtaalam |
| 15. Dr. Lucia Kafumu | - Mganga Mkuu (W) | - Mtaalam |
| 16. Bw. Yereimias Ngerangera | - Afisa Habari | - Mtaalam |
| 17. Bw. Estery Mwinuka | - Kaimu Afisa Uchaguzi | - Mtaalam |
| 18. Bw. Samson Manjale | - Kaimu Afisa Manunuzi (W) | - Mtaalam |
| 19. Bi. Virgilia Shawa | - Mtendaji wa Mamlaka M/Mdogo Lusewa | - Mtaalam |
| 20. Bi. Prisca Msuha | - Kaimu A/Ardhi na Maliasili (W) | - Mtaalam |
| 21. Bw. Abdallah Maarufu | - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) | - Mtaalam |
| 22. Bw. Hyazint Mbiro | - PSSNC TASAF | - Mtaalam |

WATAALAM WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA:-

- | | | |
|--------------------------|--------------------------------|-----------|
| 1. Bw. Hasani Kinonono | - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) | - Mtaalam |
| 2. Bi. Sekela Mwamwezi | - Mthibiti Ubora wa Shule (W) | - Mtaalam |
| 3. Bw. Revocatus Kavishe | - Afisa Biashara | - Mtaalam |

SEKRETARIETI:

- | | | |
|---------------------------|----------------------|------|
| 1. Bw. Solomon Hyera | - Mwandishi wa Vikao | - CC |
| 2. Bi. Benadetha Ndunguru | - Mwandishi wa Vikao | - CC |

KUMBU NA - NMT/FUM/08/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao, kabla ya kufungua kikao Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao na kuwaomba kujadili taarifa mbalimbali huku wakijikita zaidi katika kujadili namna ya kuboresha ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo lililopangwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kisha alifungua kikao saa 04:15 asubuhi.

KUMBU NA - NMT/FUM/09/2021/2022: KUSOMA NA KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 18/12/2021.

Wajumbe walisomewa agenda za kikao cha tarehe 18/11/2021 na baada ya kusomwa agenda, Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo kujadiliwa katika kikao hicho.

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 18/11/2021
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 18/11/2021
5. Kupokea na kujadili taarifa mapato na matumizi mwezi Novemba 2021 mwaka wa fedha 2021/2022.
6. Taarifa mbalimbali
 - A. Taarifa ya utekelezaji wa mpango mkakati wa agizo la serikali la kuwapanga wafanyabiashara wadogo (machinga).
 - B. Taarifa ya mpango wa manunuzi ya bidhaa na huduma zisizo za kishauri julai 2021 – juni 2022
7. Maombi na mabendekezo mbalimbali
 - A. Ombi la kutumia tsh 90,000,000/= ujenzi wa nyumba ya mtumishi (two in one)
 - B. Ombi la kutumia tsh 150,000,000/= umaliziaji wa maboma ya zahanati ya nahoro, namali na sasawala
 - C. Ombi la kutumia tsh 800,000,000/= kuendeleza ujenzi wa majengo katika hospitali ya wilaya
 - D. Ombi la kutumia tsh 250,000,000/= ujenzi wa kituo cha afya ligera
 - E. Ombi la kutumia fedha za mfuko wa pamoja wa uendeshaji wa huduma za afya (basket fund)
 - i. Tsh 114,496,883.17 mfuko wa pamoja wa uendeshaji wa huduma za afya (basket fund) (bf)
 - ii. Tsh 20,205,332.33 mfuko wa pamoja wa uendeshaji wa huduma za afya
8. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti.
9. Kufunga kikao

KUMBU NA - NMT/FUM/10/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO WA TAREHE 18/11/2021

Wajumbe walipitia muhtasari kwa makini na waliridhia katibu na Mwenyekiti kutia saini ili kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

KUMBU NA - NMT/FUM/11/2021/2022: KUSOMA NA KUJADILI YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 18/11/2021

- Utekelezaji wa maagizo ya awali uliwasilishwa na wajumbe wa kamati walionesha kuridhishwa utekelezaji wake, Aidha wajumbe walisisitiza korosho kuuzwa katika soko la Namtumbo
- Wajumbe walihoji juu ya Mafundi wa SWASH kama wamepata mafunzo . Pia wajumbe waliag kuandaliwa kwa taarifa ya matumizi ya fedha ya SWASH tsh 272,000,000/= Aidha wajumbe waliag kwa m iradi inayoendelea kila fedha inapo tumika taarifa yake iandaliwe na kuwasilishwa kwenye kikao cha kamati ya Fedha ili kuondoa mjadala mkubwa katika Vikao Wajumbe waliagiza kutembelea miradi ya SWASH
- Wajumbe walisimamisha kikao kwa muda na kuagiza kwenda kukagua baadhi ya miradi ya SWASH ambapo walienda mradi wa Zahanati ya Libango ambapo walikuta fundi anaendelea na kazi pia mbili iliyoezekwa ni geji 30, Litola nako walikuta bati moja geji 30 na fundi hakuwepo na Ukamilishaji nyumba ya Mganga ya Ukiwayuyu.

- Kutokana na mambo yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa miradi ya SWASH wajumbe waliagiza kuwa Mkuu wa kitengo cha manunuzi na Mkuu wa idara ya Afya kutoka nje ili kuweza kujadili miradi hiyo kwa kina Agizo hilo lilitokelezwa na kikao kikaendelea.
- Wajumbe waliagiza Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kuwachukuliwa hatua Mkuu wa kitengo cha Manunuzi na Mkuu wa Idara ya Afya na kusimama kazi mpaka maamuzi ya baraza yatakapo amuliwa Kutokana na agizo hilo Afisa sheria alitoa ufafanuzi juu ya kanuni za kudumu za Halmashauri ambapo alieleza kuwa kamati ya fedha sio mamlaka ambayo inaweza kuwasimamisha kazi watumishi isipokuwa Baraza la Madiwani
- Wajumbe waliagiza kuwa Tarehe 30/12/2021 miradi yote ya SWASH inayotekelezwa katika halmashauri iwe imekamilika Aidha walisisitiza mara baada ya tarehe 20/12/2021 kiitwe kikao cha kamati ya fedha.

KUMBU NA - NMT/FUM/12/2021/2022: KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI NOVEMBA 2021 MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

A. TAARIFA YA IDARA YA FEDHA (MAPATO NA MATUMIZI)

Taarifa iliwasilishwa ikieleza hali halisi ya ukusanyaji wa mapato na matumizi kwa kipindi mwezi Novemba 2021 baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walichangia kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

- Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipongeza ukusanyaji wa mapato na kuisisitiza juhudi za ukusanyaji kuendelea ili kufikia lengo.
- Wajumbe walihoji juu ya kituo cha mabasi Namtumbo kutokufanya kazi wakati kimekamilika Ufafanuzi ulitolewa kuwa jambo linalishughulikiwa kwa sasa ni utaratibu wa kumlipa makandalasi na ukikamilika kituo cha mabasi kitaanza kufanya kazi
- Wajumbe walihoji juu ya mkakati wa hali na mali kuhakikisha wakulima wanahamasishwa kulima na kupewa mbegu zilizo bora kwani Mkulima anachwa peke yake bila kufuatiliwa na kupewa huduma bora za ugani Ufafanuzi ulitolewa kuwa elimu imetolewa na mbegu zimetolewa kwa wakulima kulingana na mahitaji kutoka vijijini.
- Wajumbe walishauri Afisa biashara kukutana na wafanyabiashara wakubwa kuja kuwekeza katika wilaya ya Namtumbo ili kurahisisha upatikanaji wa huduma

KUMBU NA - NMT/FUM/13/2021/2022: TAARIFA MBALIMBALI

A. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI WA AGIZO LA SERIKALI LA KUWAPANGA WAFANYABIASHARA WADOGO (MACHINGA).

- Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliridhia taarifa hiyo na hawakuwa na hoja yoyote.
- B. TAARIFA YA MPANGO WA MANUNUZI YA BIDHAA NA HUDUMA ZISIZO ZA KISHAURI JULAI 2021 – JUNI 2022
- Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walihoji juu ya huduma zisizo za kishauri ufafanuzi ulitolewa na waliridhia taarifa hiyo.

KUMBU NA - NMT/FUM/14/2021/2022: MAOMBI NA MAPENDEKEZO MBALIMBALI

A. OMBI LA KUTUMIA TSH 90,000,000/= UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI (TWO IN ONE)

Halmashauri imepokea fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya idara ya afya, Hivyo idara inaomba kibali cha kutumia fedha hizo kama kiambata kinavyo jieleza

- Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walichangia kutoa maagizo na ushauri kama ifuatavyo:-
- Wajumbe walishauri baada ya kujenga nyumba ya watumishi zahanati ya Magazini ni bora nyumba hiyo ikajengwa Kijiji cha Likusanguse mahali amabapo ni mbali na makao makuu ya Kata na hakuna nyumba za watumishi Wajumbe wakamati waliridhia hoja hiyo Aidha Afisa mipango alitoa ufafanuzi kuwa fedha hizo zimekuja na miongozo hata hivyo barua zitaandikwa ilikuomba mabadiliko hayo

B. OMBI LA KUTUMIA TSH 150,000,000/= UMALIZIAJI WA MABOMA YA ZAHANATI YA NAHORO, NAMALI NA SASAWALA

Halmashauri imepokea fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya idara ya afya, Hivyo tuonaomba kibali cha kutumia fedha hizo kama kiambata kinavyo jieleza

- Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliridhia ombi hilo la kutumia tsh 150,000,000/= umaliziaji wa maboma ya zahanati ya Nahoro, Namali na Sasawala.

C. OMBI LA KUTUMIA TSH 800,000,000/= KUENDELEZA UJENZI WA MAJENGO KATIKA HOSPITALI YA WILAYA

Halmashauri imepokea fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya idara ya afya, Hivyo tuonaomba kibali cha kutumia fedha hizo kama kiambata kinavyo jieleza

- Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walichangia kutoa maagizo na ushauri kama ifuatavyo:-
- Wajumbe walishauri kutumia Mkandarasi na sio Force account Ufafanuzi ulitolewa na Afisa maipango kuwa kwa sasa hakuna muongozo ulitolewa na serikali juu ya kutumia Mkandarasi katika miradi hiyo
- Wajumbe walikubaliana na wataalam juu ya kutumia Force account katika ujenzi wa majengo ya Hospitali wajumbe walisisitiza majengo kuwa na ubora
- Aidha wajumbe waliridhia ombi la kutumia tsh 800,000,000/= kuendeleza ujenzi wa majengo katika hospitali ya wilaya huku wakisisitiza mradi kukamilika kwa wakati na kwa ubora.

D. OMBI LA KUTUMIA TSH 250,000,000/= UJENZI WA KITUO CHA AFYA LIGERA

Halmashauri imepokea fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya idara ya afya, Hivyo tuonaomba kibali cha kutumia fedha hizo kama kiambata kinavyo jieleza

- Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walichangia kutoa maagizo na ushauri kama ifuatavyo:-
- Wajumbe walikubaliana na ombi la kutumia tsh 250,000,000/= ujenzi wa kituo cha afya Ligera pia walisisitiza kuhakikisha ubora unakuwepo katika ujenzi wa majengo.

KUMBU NA - NMT/FUM/15/2021/2022: OMBI LA KUTUMIA FEDHA ZA MFUKO WA PAMOJA WA UENDESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA (BASKET FUND)

A. TSH 114,496,883.17 MFUKO WA PAMOJA WA UENDESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA (BASKET FUND) (BF)

B. TSH 20,205,332.33 MFUKO WA PAMOJA WA UENDESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA

- Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliridhia ombi hilo kama lilivyo wasilishwa huku wakisisitiza kuhakikisha huduma zinatolewa kwa wananchi vizuri


KUMBU NA - NMT/FUM/16/2021/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.

- Wajumbe walihoji juu ya Tsh 6,000,000/= iliyotengwa kwaajili ya mafunzo ya mafundi imepelekwa wapi Je mafunzo walipewa au hawakupewa na fedha hiyo imetumika kwaajili ya nini Ufafanuzi ulitolewa kuwa ni vyema taarifa yake ikaletwa katika kikao baini kama imetumika imefanya kazi gani.
- Wajumbe walihoji kwanini Kamati ya fedha haijaenda kutembelea ujenzi wa madarasa 86 ya miradi ya UVIKO –19 Ufafanuzi ulitolewa na Afisa Mipango kuwa ilionekana waheshimiwa Madiwani wananguvu ndio maana wakaombwa kubaki katika kata zao Wajumbe waliagiza kuwa wiki ijayo iandaliwe ratiba kwaajili ya kukagua miradi ya mapambano dhidi ya UVIKO – 19
- Wajumbe waliagiza Mkaguzi wa ndani kuhakikisha anakagua miradi yote ya Ujenzi wa miundombinu ya Mapambano dhidi ya UVIKO – 19

- Wajumbe walihoji juu ya kuanzishwa chama kikuu cha ushirika katika Wilaya ya Namtumbo ufafanuzi ulitolewa na Afisa Ushirika kuwa wajumbe wa SONAMCU ambao wengi ni kutoka Namtumbo wajenge hoja ngazi ya vyama vya msingi na kuipeleka katika chama kikuu
- Marejesho ya mikopo ya kilimo wakopaji wamelalamika kuambiwa kurejesha kuanzia mwezi wa tatu muda ambao sio wa mavuno Ufafanuzi ulitolewa kuwa muongozo unaeleza kuwa mkopaji atapewa muda wa miezi mitatu ndipo aanze kurejesha Pia kama kutakuwa na shida mkopaji atoe taarifa mapema ili kuondoa matatizo yanayoweza jitokeza kwa mkopaji..

KUMBU NA - NMT/FUM/17/2020/2021: KUFUNGA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao, kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti alihimiza yote yaliyoagizwa katika kikao hicho kufanyiwa kazi kwa wakati Aidha aliongeza kuwa miradi yote kufikia tarehe 30/12/2021 iwe imekamili Pia alipongeza kukamiliika kwa wakati ujenzi wa miundombinu ya ujenzi wa madarasa 86 ya mapambano ya UVIKO -19, Kamati ya fedhha ikakague miradi kuanzia tarehe 30/12/2021 Mwenyekiti aliwataka wataalam kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele kuwaongoza waheshimiwa madiwani katika kusimamia maendeleo ya Halmashauri kisha alifunga kikao saa 10:45 Mchana.



.....
SAINI YA KATIBU

UMETHIBITISHWA,



.....
SAINI YA MWENYEKITI

TAREHE 16/02/2022.